# KISWAHILI, USAMBAZAJI WA HABARI NA UHAMASISHAJI WA UMMA KWA AJILI YA MAENDELEO

***E.S. Mohochi***

**Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro, Kenya**

**Ikisiri**

*Umuhimu wa kimsingi wa maendeleo ni kupatikana kwa hali bora ya maisha kwa jamii nzima. Haitoshi kuzungumiza maendeleo iwapo yanawanufaisha wachache na kuacha wengi katika hali ya uchochole. Ili kuyafikia hayo maendeleo muafaka, ni muhimu kuwashirikisha wananchi wote katika maamuzi na utekelezaji wa sera mbalimbali zinazofikiwa kwa minajili ya kuleta maendeleo katika jamii. Si hilo tu bali hata yale yanayoamuliwa na viongozi wao yanapaswa kuwasilishwa kwao kwa lugha watakayoielewa vyema. Tutakapofaulu kufanya hivyo, tutawapa wananchi fursa ya kuhisi kuwa harakati hizo ni za wananchi wote na watashiriki bila kuwashuku wachache wanaotoa maamuzi na maagizo huku wao wakitarajiwa kuyapokea na kuyatekeleza bila maswali.*

*Lengo hili laweza kufikiwa kwa kukuza mfumo mwema wa mawasiliano baina ya asasi mbalimbali za serikali na za kibinafsi na umma kwa jumla. Mfumo kama huo utatuwezesha kukuza njia nzuri ya usambazaji wa habari muhimu kwa wote pamoja na uhamasishaji wa umma ili ushiriki katika juhudi za kuboresha hali ya maisha nchini. Ingekuwa vyema zaidi kama tungewafikia watu katika lugha zao mbalimbali wanazozielewa zaidi, lakini hilo litachukua muda zaidi. Kwa bahati nzuri tunayo lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka na wengi katika eneo hili la Afrika Mashariki na Kati. Ni azma ya makala haya kuonyesha nafasi muhimu ambayo lugha ya Kiswahili yapaswa kupewa katika vyombo vya habari ili kutuwezesha kuyafikia malengo yetu ya maendeleo kwa kurahisisha mawasiliano. Kwa sasa, lugha hii imenyimwa fursa ya kufanya hivyo.*

## UTANGULIZI

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya serikali, ni lile la kuongoza jitihada za maendeleo katika jamii. Maendeleo nayo yamenuiwa kuiboresha hali ya maisha ya wananchi na serikali inapaswa kuyadhibiti kwa kuongoza mkondo wake. Serikali hulitekeleza hili kwa kupitia idara zake mbalimbali ambazo hufanya kazi pamoja na asasi zingine zisizo za kiserikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma muhimu wanazostahili. Wakati huohuo, ni sharti serikali

ihakikishe kuwa kuna mazingira mema yatakayo wawezesha wananchi kutoa mchango wao kwa kushiriki katika jitihada za kuinua hali zao za maisha.

Kwa mantiki hiyo, maendeleo ya jamii yanahitaji muafaka wa aina fulani ambao utauwezesha kila upande kutoa mchango wake ili juhudi za pande zote zielekezwe katika kulifikia lengo moja. Muafaka huo hauwezi kufikiwa pasipokuwa na mfumo mzuri wa mawasiliano utakaohakikisha kwamba maamuzi mbalimbali yafanywayo katika nyanja kadha wa kadha za maisha yanawasilishwa kwa wote yatakaowaathiri. Ni lazima umma ufahamu sera zilizofikiwa, namna zitakavyowagusa, matatizo yaliyopo na matarajio ya baadaye. Mawasiliano ya aina hiyo yatauandaa umma kuwa tayari kujitoa muhanga huku ukijua kuwa huko waelekeako kuna afueni. Njia nzuri ya kutumiwa kuufikia huo mfumo muafaka wa mawasiliano ni kwa kupitia vyombo vya habari. Makala haya yanachunguza matumizi ya vyombo vya habari katika usambazaji wa habari muhimu kwa umma kwa kuzingatia lugha itumiwayo katika hivyo vyombo vya habari.

## Vyombo vya Habari na Usambazaji wa Habari

### *Usuli wa Vyombo vya Habari*

Uwezo wa kuwasiliana, hasa kwa kutumia lugha katika mazungumzo au maandishi, ni sifa moja muhimu sana inayowaweka binadamu katika daraja tofauti na wanyama wengine. Kwa maana hiyo, binadamu amekuwa akiwasiliana na wenzake tangu jadi. Jamii tofauti zimekuwa na mifumo yao ya mawasiliano lakini kadri ya mabadiliko yanavyoikumba jamii, mifumo hiyo inabadilika na kuboreshwa. Kutokana na maendeleo ya mifumo ya mawasiliano, vyombo vya habari vimeleta mabadiliko makubwa sana ulimwnguni; la muhimu zaidi likiwa uwezo wa kupitisha ujumbe kwa mamilioni ya watu kwa wakati mmoja. Kimsingi; vyombo vya habari vimegawika katika makundi mawili makuu: kundi la uchapishaji na lile la utangazaji (Harris, 1989). Vyombo vya habari vya uchapishaji hujumuisha majarida, magazeti, vitabu, n.k. ilhali vya utangazaji (elektroniki) ni pamoja na radio, televisheni, sinema, n.k.

Vyombo vya habari, katika hizo sura zake mbalimbali, vina historia ndefu sana. Kulingana na Barry et al. (1965), gazeti la mwanzo kabisa la kila siku, "The London Daily Courant" lilianzishwa mnamo mwaka wa 1702. Kwa upande wa vyombo vya habari vya elektroniki, mbinu za kutengeneza picha hai na kutuma sauti zilivumbuliwa kuelekea mwishoni mwa karne ya 19. Matangazo ya mwanzo ya habari yalifanyika 1916 na yalihusu matokeo ya uchaguzi wa uraisi wa Marekani (Barry et al., 1965). Utangazaji wa radio uliimarika vizuri katika jamii ya Marekani baina ya miaka ya 1920 na 1930 (Oskamp, 1991).

Juhudi za awali za kuonyesha picha hai pamoja na sauti zilifanywa mwaka 1925 na John Logie Baird. Miaka miwili baadaye C.F. Jenkins, mhandisi wa "Bell Telephone Company" akazalisha picha za mwanzo kuonekana katika televisheni nchini Marekani. Televisheni kama tuijuavyo hivi leo ilishamiri katika miaka ya 1940 na katika mwaka wa 1953, Marekani ikazindua mtambo wa mwanzo kabisa wa televisheni ya rangi (Barry et al., 1965). Tangu wakati huo hadi sasa, vyombo vya habari vinaendelea kutekeleza majukumu mbalimbali muhimu katika jamii.

**Umuhimu wa Vyombo vya Habari**

Umuhimu wa vyombo vya habari unadhihirika bayana tunapoyachambua majukumu yake mbalimbali katika jamii. Kama vifaa vya mawasiliano, vyombo vya habari vinatoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya umma. Kwa jumla, vyombo vya habari hutumika kuelimisha, kuburudisha na kufahamisha. Tunafahamishwa mengi ya kila siku katika nyanja mbalimbali za maisha kutokana na shughuli za vyombo vya habari. Mawasiliano ya vyombo vya habari hututembeza kwingi katika shughuli za kisiasa, kidini, kielimu, kijamii n.k. Aidha, vyombo vya habari ni vyanzo maridhawa vya burudani tunayoihitaji kujipumzisha na kuajiliwaza baada ya uchovu utokanao na hali ngumu ya maisha. Vyombo vya habari hufunza kuliko mwalimu yeyote kwa sababu ya ukubwa wa hadhira yake pamoja na upana wa maswala vinayoyazingatia. Hata hivyo, mgao wa majukumu ya vyombo vya habari katika makundi matatu ya kufahamisha, kuburudisha na kuelimisha ni wa jumla mno na hautufunulii waziwazi matumizi yake mengi katika jamii. Yafuatayo ni baadhi tu ya matumizi mahsusi ya vyombo vya habari katika jamii.

Vyombo vya habari vina nguvu na msukumo mkubwa sana katika maisha ya kila siku ya jamii. Kutokana na sifa hizo, vinaweza kutumika kujenga na kuendeleza matarajio na mielekeo ya pamoja ya jumuia (Barry et al.; 1965). Wakati huohuo, vitasaidia kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, mienendo, na mavazi ya watu, n.k. au pia kuongoza uvumbuzi katika jamii na kuingiza mienendo mipya kutoka tamaduni tofauti. Kwa vile vinagusa hali mbalimbali za maisha yetu, vyombo vya habari vinaweza kutumika vizuri sana kama vifaa vya kushawishi watu na kuongoza mabadiliko yafaayo katika jamii.

Kuongezeka kwa idadi ya vyombo vya habari na umiliki wa vyombo hivyo miongoni mwa watu kwa pamoja kumewezesha kuvipa nguvu zaidi. Vinawafikia watu wengi (mamilioni kwa mamilioni) kwa wakati mmoja. Hali hii inafafanuliwa zaidi na Barry et al. (1965: 264).

> Funzo lolote litolewalo katika sinema, radio ama televisheni huweza kuwafikia mamilioni ya watu kwa kuvuka mipaka ya kutojua kusoma

na kuandika na kuwawezesha waliotengwa kuelewa mambo muhimu.

Nao McQuail (1987) na Wood (1983) wanatueleza kuwa vyombo vya habari hutumika kutambua, kufuata na kueleza matukio mbalimbali katika mazingira yetu, hasa kwa kuyahusisha na hali ya kisiasa na kiuchumi inayotawala maisha yetu. Aidha, vinatoa fursa kwa watu wengi kujihusisha na kushiriki katika maamuzi na majadiliano kuhusu masuala tofauti yanayoathiri maisha yao kitaifa na kimataifa. Swali la msingi tunalouliza ni kama vyombo vyetu vya habari vinatumiwa ipasavyo kulifikia lengo hilo.

### *Umuhimu wa Habari Pamoja na Usambazaji Wake Katika Jamii*

Jamii zote, tangu Babylon hadi leo, zimeumbwa kutokana na uwezo wa kuzalisha na kusambaza habari (Innis, Dicard 1982). Maendeleo yetu kiuchumi, kisayansi, kijamii n.k. yamewezekana kwa sababu ya uwezo wetu wa kuwasiliana. Hata hivyo, mifumo ya mawasiliano inatofautiana katika jamii mbalimbali. Miongoni mwa mengine, tofauti hizo ni matokeo ya maendeleo katika teknolojia za mawasiliano. Baadhi ya jamii zina vyombo vya kisasa vya mawasiliano ambavyo vinarahisisha upashanaji wa habari miongoni mwa watu wengi zaidi. Kwingineko vifaa hivyo vipo lakini kiwango cha umaskini katika jamii hizo hakiruhusu watu wengi kuvimiliki. Hali hizi zote zinakwaza sana juhudi za kutaka kuelimisha umma.

Hivi sasa ulimwengu uko katika enzi ya teknolojia ya habari kwa sababu ya umuhimu mkubwa ambao habari inashikilia katika maisha yetu. Dicard (1982) anafafanua utabiri uliotolewa awali na Arnold Tonybee kuwa karne ya ishirini itamwezesha binadamu kuyaangaza maslahi ya binadamu wengine wote ulimwenguni kwani mawasiliano mapana ya elektroniki yatamwezesha kufahamu yanayoendelea kila mahali. Naye Deutsch (Dicard, 1982) anasema kwamba habari ni nguvu, na katika jamii inayoendelea kiteknolojia umiliki na udhibiti wa upataji wa habari utakuwa muhimu kuliko udhibiti wa polisi na majeshi mengine. Umuhimu huu wa habari unaendelea kuwa mkubwa zaidi kila siku. Umuhimu na nguvu hii husababisha tawala mbalimbali kutaka kumiliki na kuongoza vyombo vya habari ili kuchuja yanayowafikia wananchi. Barry et al. (1965: 26), wanadai kuwa umiliki wa vyombo mbalimbali vya habari umekuwa silaha ya kisiasa iliyo na umuhimu sawa na umiliki wa jeshi na polisi. Wanafafanua hoja hiyo kama ifuatavyo:

> Kwa sababu ya ukubwa wa hadhira yake, radio, televisheni, filamu na magazeti huweka nguvu nyingi na wajibu mkubwa sana mikononi mwa wale wanaovimiliki. Mara nyingi uwezo huu hutumika kwa manufaa ya kisiasa na kifedha. Huwawezesha wamiliki kuzuga watu wasio na elimu ya kutosha. Malengo haya yote hufikiwa kwa kuelemea upande mmoja

maalum wakati wa uteuzi na uwasilishaji wa mambo, kwa uongo wa wazi, ama kwa kuchezea shauku na matarajio ya hadhira.

Walio na nyadhifa za uongozi hutumia sana vyombo vya habari kuyafikia malengo haya zaidi katika jamii ambazo zina idadi kubwa ya umma usiokuwa na ufahamu mpana wa matukio yanayowazunguka. Kwa bahati mbaya hali hii ndiyo inapatikana katika nchi nyingi barani Afrika na kwingineko katika ulimwengu wa tatu.

Kumeibuka mabadiliko makubwa katika jamii na teknolojia ya mawasiliano inatawala nyanja zote za maisha yetu kwa sasa. Katika hali tuliyo nayo, maendeleo na ubora wa maisha ya baadaye unategemea uwezo wa kumiliki, kuhifadhi, kuchanganua na kuwasilisha habari. Lyon (1988) anarejelea ripoti ya Kitaifa ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Wingereza inayosema kuwa kuchelewa kuchukua mkondo huo kwaweza kuifanya nchi iliyoendelea kuwa sawa na nchi za ulimwengu wa tatu. Kasamu (1996) na Lumumba (1997), wanaliendeleza wazo hilohilo kwa kusema kuwa habari ni nguvu na kama vile, mtaji na malighaji nyingine, ni raslimali ya kimsingi sana katika maendeleo ya viwanda. Kwa upande wake, Toffler (Lyon, 1988) anasema kuwa suala zima la umuhimu wa habari limetufikisha katika wimbi la tatu la maendeleo ya ulimwengu. Wimbi la kwanza lilikuwa la kilimo na la pili likawa lile la viwanda. Wamarekani wanajivuna kwani wao, katika maendeleo ya jamii, wameshapita hatua ya ustaarabu wa kilimo, ustawi wa viwanda na sasa jamii yao inasisitiza uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa habari. Kwa maana hiyo, wako katika wimbi la tatu la maendeleo.

Aidha, habari sasa inachukuliwa kama bidhaa inayouzwa. Katika hali hiyo, umiliki wa bidhaa hii muhimu unampa anayeimiliki uwezo mkubwa sana; uwezo ambao unaendelea kuongezeka siku baada hadi siku (Lyon, 1988). Aliye na bidhaa hii ana uwezo wa kuchagua la kusambaza na la kubania; pamoja na nguvu kwa sababu yeye anaelewa ambayo wengine hawayaelewi. Ana ufahamu zaidi. Kwa wakati huu, habari ni bidhaa inayouzika sana na ndiposa kampuni na watu binafsi wanagombania fursa ya kuekeza katika biashara ya teknolojia ya habari katika sura zake mbalimbali. Kwa upande wa hadhira, kuna umuhimu mkubwa sana kwao kupata bidhaa hii kutokana na ukweli kwamba umma ulio na fahamu utaweza kufanya maamuzi muafaka kuhusu masuala mbalimbali maishani, tofauti na umma ulio gizani.

Katika nchi zilizoendelea, ambapo takribani kila mtu mzima anajua kusoma na kuandika, kila mtu husoma gazeti la kila siku, au sehemu tu ya gazeti hilo ingawa baadhi hawasomi vitabu kamwe (Barry et al. 1965). Barry et al. (1965) wanaendelea kusema kwamba kuna zaidi ya magazeti 8000 yachapishwayo kila siku kote ulimwenguni. Naamini kwamba kufikia sasa idadi hiyo imeongezeka,

si haba. Kwa bahati mbaya, nchi nyingi zinazoendelea hazina idadi kubwa ya watu wanaojua kusoma na kuandika, na kutokana na hali hiyo, magazeti hayatekelezi jukumu kubwa sana kama vyanzo vya habari kwao. Kwa hiyo wengi huiona radio, wanayoitumia kwa kiasi kikubwa, kama mlango muhimu unaowafunulia yanayoendelea nchini na kwingine duniani.

Kuhusu suala hilohilo la athari kuu ya vyombo vya habari katika maisha yetu, McCombs (Oskamp, 1991) anasema kwamba huenda athari muhimu zaidi ya vyombo vya habari kwa umma ni katika jukumu lake la kuibua na kuongoza ajenda ya majadiliano katika jamii. Yanayopokelewa kupitia vyombo vya habari huzingatiwa kwa makini sana na wasikilizaji au watazamaji na wasomaji ambao huyajadili kwa mapana na kuyachuja. Kwingineko, Oskamp (1991: 167) anayafafanua mawazo ya Kinder & Sears, na Roberts & Maccuby kwa kusema hivi:

> ...Hata hivyo, vyombo vya habari havipitishi habari tu. Kwa kuteua, kusisitiza na "kutathamini" matukio mahsusi na kwa kutangaza mwitikio na mchango wa umma kuhusu matukio hayo, vinasaidia kuunda umbo la hali halisi na kutambulisha mambo muhimu ya wakati huo. Hali hii ina matokeo ya kuufanya umma kujenga mielekeo maalum kuhusu masuala hayo.

Kwa hakika, vyombo vya habari vina nguvu nyingi sana za kuongoza mkondo wa mawazo ya umma kuhusiana na mambo mbalimbali.

**Hali Katika Vyombo vya Habari Nchini Kenya**

Baada ya kuweka bayana umuhimu mkubwa wa habari katika jamii hivi sasa ulimwnguni, pamoja na nafasi muhimu ya vyombo vya habari kama vyanzo vya habari hizo, ni muafaka sasa kuigeukia hali halisi hapa nchini. Tumeona kuwa vyombo vya habari vina matumizi na manufaa kadha wa kadha katika jamii. Miongoni mwa majukumu yake muhimu ni kuuwezesha umma kushiriki katika mijadala ya mambo muhimu yanayoathiri maisha yao kila siku. Hali ilivyo hapa nchini ni kwamba vyombo vya habari havijauwezesha umma kuwa mshiriki muhimu katika maendeleo ya hali zao. Nini sababu ya hali hiyo?

**Vyombo vya Habari vya Maandishi**

Kwanza kabisa, idadi kubwa ya Wakenya haijui kusoma na kuandika. Kwa hivyo, magazeti ambayo hubeba maelezo kuhusu mambo mengi mbalimbali tena kwa kina kirefu yako nje ya upeo wao. Wanalazimika kuitegemea radio na televisheni ambazo vilevile zinadhihirisha udhaifu mkubwa kwa kupendelea lugha isiyoeleweka na wengi. Kulingana na Sure, akinukuliwa na Adegbija (1994: 50), takribani asilimia 50 ya Wakenya huzungumza Kiswahili, japo

viwango vyao vya uelewa wa lugha hiyo vinatofautiana sana. Hali ni kinyume kuhusu Kiingereza ambapo idadi inayokielewa haizidi 5%. Mberia (2000) anarejelea utafiti uliofanywa 1980 unaokadiria wazungumzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Kenya kuwa 65.3% huku wa Kiingereza wakiwa 16.1%. Japo viwango hivi vinatofautiana, jambo lililo wazi ni ukweli kuwa lugha inayoeleweka na wengi ni Kiswahili. Adegbija (1994) anasema kwamba hivyo ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za Afrika kuhusu lugha za kienyeji na zile za kikoloni.

Kwa kuzingatia ukweli huo, inasikitisha sana kuona kuwa vyombo vingi vya habari bado vinatumia zaidi lugha za kigeni na hivyo kuwaacha gizani wananchi wengi. Kwa upande wa magazeti, lipo gazeti moja tu la Kiswahili la kila siku hapa nchini. Machache yaandikwayo kwa lugha nyingine za Kiafrika huchapishwa baada ya muda na wakati mwingi huacha uchapishaji kipindi kifupi tu baada ya kubuniwa. Kiganya (Mlacha, 1995) anatudokezea ripoti ya "Audit Bureau of Circulation" (ABC) ya Machi na Aprili 1989. Katika kipindi hicho, nakala 267,750 za magazeti ya Kiingereza zilisomwa kila siku kati ya Jumatatu na Jumamosi zikilinganishwa na nakala 56,975 za magazeti ya Kiswahili. Bila shaka takwimu hizo ni tofauti sana wakati huu lakini la msingi ni kwamba, kwa vile wengi wanailewa lugha ya Kiswahili na wala si Kiingereza ni bayana kwamba idadi kubwa ya Wakenya haizifuatilii habari za kila siku kupitia magazetini. Ni kweli kwamba gazeti la *Taifa Leo* lina upungufu lilinganishwapo na gazeti la *Nation*, lakini hiyo siyo sababu kuu inayotupatia takwimu hizo. Isitoshe, majarida mbalimbali yanayofafanua taaluma kadha wa kadha na kuripoti matokeo ya tafiti katika nyanja mbalimbali huandikwa kwa Kingereza. Vilevile bali hata makongamano mengi yanayohusiana na mambo muhimu maishani mwetu hufanywa kwa Kiingereza kisha mahitimisho na mapendekezo yao pia kuchapishwa kwa lugha hiyohiyo ambayo, kama tulivyokwisha kutaja, haimilikiwi na wengi wetu.

**Vyombo vya Habari vya Elektroniki**

Vyombo vya habari vya elektroniki vina nafasi kubwa zaidi ya kuwafahamisha wananchi wengi kwa sababu vinawafikia wengi kwa wakati mmoja. Aidha, idadi kubwa ya watu hupata fursa ya kuvisikiliza na pia kuvitazama. Hata hivyo, katika kundi hilo, radio ndiyo ipatikanayo katika sehemu nyingi zaidi za nchi.

**Radio**

Japo, kutokana na umaskini uliopo nchini, baadhi ya familia hazina radio, aghalabu chombo hiki hupatikana hata katika sehemu za mashambani. Kijiji kizima hakikosi angalau radio moja ambayo watu wote huweza kuizingira na kufuatilia matukio muhimu nchini na kote ulimwenguni. Mintarafu ya hilo,

radio ni chombo muhimu sana cha uelimishaji na uhamasishaji wa umma. Tangu kuanzishwa hapa nchini mwaka 1927, ikiwa ya pili barani Afrika, radio imeendelea kuwa kifaa cha pekee cha mawasiliano baina ya serikali na umma, licha ya mabaraza ya viongozi wa mashinani.

Ingekuwa bora zaidi kutumia lugha zetu mbalimbali kuwasiliana na wasikilizaji lakini idhaa zinazotumia lugha zetu za kwanza hurusha matangazo kwa saa chache sana na haziwezi kuyashughulikia mambo mengi tofautitofauti. Katika hali hii, radio ambayo ingewafaa wengi zaidi ni KBC – idhaa ya Kiswahili kwani lugha hii inaeleweka na wengi. Kinyume na matarajio hayo uchunguzi wetu unaonyesha kwamba idhaa hii imeelemea zaidi vipindi vya salamu na burudani ya muziki. Idadi kubwa ya vipindi vinavyowasilisha sera mbalimbali muhimu na kuyajadili matukio mengi yahusuyo maisha yetu ya kila siku hupatikana katika idhaa ya Kiingereza. Kwa mfano, wakati wa uchaguzi wananchi wanahitaji kupata fursa ya kuwasikia wagombea mbalimbali wakijieleza ili watoe maamuzi muafaka. Hatupati fursa hiyo kwani mambo mengi muhimu kama hayo yanaendeshwa kwa Kiingereza. Mipango mbalimbali ya utayarishaji wa uchaguzi uliofanyika mwaka 1997 kama vile; uandikishaji wa wapiga kura, pamoja na vipindi vingi vilivyowasilishwa kuhusu maandalizi hayo vilifanywa kwa Kiingereza. Hali ni hiyohiyo katika matayarisho ya uchaguzi wa mwaka huu (2002). Maandalizi mengi na maelezo kuhusu sensa ya mwaka 1999 yalitolewa katika lugha ya Kiingereza. Suala la mipango ya urekebishaji au uandalizi wa katiba mpya pamoja na mjadala wote ambao umekuwepo nasi kwa muda sasa umefanyika zaidi kwa lugha ya Kiingereza. Barry et al. (1965: 264) anasema yafuatayo:

> Katika miongo michache iliyopita filamu na radio vimetumika sana kuelimisha jamii zisizojua kusoma na kuandika kuhusu mambo kadha wa kadha; kuanzia kujifunza kusoma hadi kwa namna nzuri za kuendesha shughuli zao za kilimo.

Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa lakini sivyo ilivyo hapa nchini na kwingineko barani. Kutokana na hali hiyo ya kutowaelimisha watu wetu, sasa tunazungumza kuhusu kina 'Wanjiku' (wananchi ambao hawakusoma wasioelewa kinachoendelea katika jamii) tunaodai hawawezi kutoa mchango wowote katika masuala ya kitaifa kwa sababu hawaelewi kitu. Ni jukumu letu kuwaelimisha badala ya kuendelea kuwaacha ushenzini. Suala la ajali barabarani limetusumbua sana hapa nchini. Jitihada nyingi zinafanywa kuhakikisha kuwa kuna hali ya usalama barabarani na miongoni mwa jitihada hizo ni kuandaa vipindi maalum kuhusu suala hilo. Moja kati ya vipindi hivyo ni kile cha "Road Carnage" cha kila wiki katika idhaa ya Kiingereza ya KBC. Je, wasafiri wa kawaida wanelewa yasemwayo? Makosa kama haya ndiyo yanayosababisha

ukosefu wa ufahamu kuhusu mambo kadha wa kadha. Kipindi cha "Legal Advisor" ni muhimu sana kwani kinaeleza, kwa lugha ya kawaida, maswala magumu ya kisheria. Ingefaa zaidi kama kingeendeshwa kwa Kiswahili pia ili wengi wayafahamu hayo.

Mfumo wa uwasilishaji wa vipindi katika radio umebadilika sana. Kumeibuka mtindo wa mawasiliano unaowashirikisha wasikilizaji kwa kupiga simu na kwa kiasi kuandika barua. Mfumo huu umetia fora sana baada ya kuiweka huru sekta ya utangazaji, hali iliyozaa vituo vingine vingi vya matangazo. Osoro (2000) anasema kuwa mtindo huu umejitokeza kwa mkupuo na kutokea kupendwa sana hasa baada ya miaka ya 90 kulipoanzishwa radio kadhaa za kibinafsi. Vipindi hivi ni vizuri na vimetokea kuwa maarufu sana kwa sababu vinatoa fursa kwa watu kueleza matatizo, hisia na matarajio kuhusu masuala mbalimbali yanayowakabili. Tunapata kusikia na kubadilishana mawazo na wananchi wa matabaka mbalimbali na kuelewa kwa jumla msimamo wa umma kuhusu yale yanayojadiliwa. Vipindi hivi vinapatikana katika radio zote hapa nchini lakini zaidi katika hizo radio mpya ambazo zimesajiliwa. Nation FM ina vipindi kama vile; "Your Shout" pamoja na "Changamka". Metro FM ina; "Let's Chat"," Metro Iove Zones", "Ladies Night" na kadhalika. Vipindi hivi hujadili mambo tofauti muhimu sana katika nyanja za siasa, uchumi, maswala ya jamii n.k.

Ubunifu huo wa radio za kibinafsi umeichemsha Kenya Broadcasting Corporation, nayo ikaanzisha vipindi kama hivyo. Tatizo ni kwamba vipindi hivyo vinasikika zaidi katika idhaa ya Kiingereza na kwa kiasi tu katika idhaa ya Kiswahili. Mifano ni pamoja na "Your Views on Phone, "Youth Variety Show", pamoja na kipindi cha "Ties that Bind". Vipindi hivyo ni vizuri sana kwa vijana kwani huwapa fursa kupiga simu na kueleza matatizo na tajriba zao kuhusu masuala mbalimbali. Aidha, wanapata pia mwongozo kutoka kwa wataalamu radioni. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo hujadiliwa katika vipindi hivi ni mimba miongoni mwa vijana, magonjwa ya zinaa na ukimwi, tatizo la madawa ya kulevya, uhusiano baina ya wazazi na watoto wao, n.k. Haya yote ni mambo ambayo yanatatiza sana vijana wa siku hizi.

Idhaa ya Kiswahili bado iko nyuma sana katika mfumo huu. Vichache vilivyopo haviwasilishwi vizuri na mada zinazomulikwa si za msingi sana. Hivi ni pamoja na "Sema Usikike", pamoja na "Umemchagua nani". Radio nyingine inayotumia lugha ya Kiswahili ni Radio Citizen ambayo ina vipindi vingi sana vinavyoelimisha umma kuhusu maamuzi ya kisiasa, n.k. Wakati huu wa kampeni za kisiasa, radio hiyo huwaalika wagombea mbalimbali wa viti kwa mahojiano radioni, pamoja na kutoa nafasi wananchi kupiga simu na kuwauliza maswali. Kwa bahati mbaya radio hii haisikiki kote nchini.

Ni wazi kwamba radio haitumikii umma vilivyo kwa kuushirikisha katika masuala muhimu nchini. Sababu kuu ni kwamba lugha inayopendelewa ni Kiingereza. Sababu ya pili ni kwamba radio inayozungumza lugha ya Kiswahili, inayoeleweka zaidi, imebaki nyuma sana katika ubunifu wa uwasilishaji wa vipindi. Isitoshe, radio ya pili kutumia Kiswahili, Radio Citizen, hairushi matangazo nchini kote. Itabidi Idhaa ya Kiswahili ifanyiwe marekebisho hima. Wakati huohuo, serikali iruhusu radio binafsi zirushe matangazo yake kote nchini kwani kwa wakati huu, manufaa ya hivyo vipindi vingi tulivyovitaja ni kwa watu wa mijini tu, hasa jijini Nairobi. Inapasa pia kuwe na sheria itakayovihitaji vituo hivyo vya binafsi kulazimika kuwa na asilimia fulani ya vipindi kwa lugha ya Kiswahili.

**Televisheni**

Hali katika televisheni hapa nchini si tofauti sana na ile tuliyoiona kuhusu radio. Kwanza kabisa, televisheni inayowafikia watu katika sehemu zote nchini ni moja tu ya shirika la utangazaji la KBC. Hata hivyo ni idadi ndogo sana ya wananchi inayomiliki runinga hasa katika sehemu za mashambani. Runinga ya KBC huwasilisha habari, matangazo ya biashara na vipindi vingine mbalimbali kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza. Licha ya habari, mambo mengine yote yanajitokeza zaidi katika lugha ya Kiingereza. Matokeo ya mfumo huu ni kwamba ni idadi ndogo tu ya watazamaji inayoyaelewa hayo.

Vipindi vingi sana vya mijadala huwasilishwa na runinga ya KBC kila juma. Vipo ambavyo ni vya kila juma na wakati mwingine mijadala maalum huonyeshwa kunapoibuka suala muhimu katika jamii. Kwa jumla mijadala hiyo huranda katika nyanja mbalimbali za maisha na ina manufaa makubwa sana kwa umma. Tatizo ni kwamba imeandaliwa kwa lugha ya Kiingereza ambayo, japo hatutaki kukubali, wengi hatuielewi. Mifano ya vipindi kama hivyo ni pamoja na; "Insight", "Face to Face", "The Debate", "Professional View", "Press Conference", "Economic Focus" na kadhalika. Aidha, wakati huu wa maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu vipo vipindi kadhaa uchaguzi. Hivi vinajumuisha: "Election Countdown", "The Third Opinion", "The Summit", n.k. Hivi ni vipindi vizuri sana kwani huwaalika wanasiasa na wataalamu wengine wa mambo ya siasa katika mijadala inayowapa wananchi ufahamu wa kuwawezesha kufanya uchaguzi mzuri wa viongozi. Tatizo ni kuwa mijadala hii na mingine kuhusu masuala mengine muhimu hufanyika katika lugha ya Kiingereza. Kwa mfano, kuna maana gani kualika watu kwenye televisheni na kujadili mambo muhimu kuhusu kilimo cha mahindi, kahawa, chai n.k. kwa lugha ya Kiingereza ilhali tunafahamu kuwa wakulima wengi hawaelewi lugha hiyo?

Televisheni mbalimbali ambazo zimeanzishwa, nyingi zikiwa Nairobi tu, zina vipindi mbalimbali vya namna hii lakini nazo pia zinatumia Kiingereza na hivyo kuwabagua wasiojua lugha hiyo. Mfano ni runinga ya Nation ambayo ina kipindi cha "Up Clopse and Candid". Mbona kuna uhaba wa vipindi kama hivi katika lugha ya Kiswahili? Wakati mmoja kulianzishwa kipindi cha "Hili na Lile, Hapa na Pale" lakini kikatoweka baada ya muda mfupi. Aidha, kipindi cha "Mjadala" huibuka na kupotea bila maelezo yoyote. Hali iliyo hapa nchini ni kwamba vyombo vya habari havitekelezi jukumu lake la msingi la kuelimisha na kufahamisha umma ili uweze kushirikishwa katika mambo mbalimbali yanayoathiri maisha yake. Kuhusu suala la lugha muafaka kutumika kuendeshea shughuli muhimu katika jamii, Kellman, akinukuliwa na Adegbija (1994:3) anasema:

> … lugha hiyo lazima itoe nafasi sawa kwa makundi mbalimbali kuhusiana na mfumo tawala na kushiriki katika mfumo huo. Kwa wakati huu, barani Afrika, ni lugha za kimagharibi zinazotumika katika hali hizo. Mintarafu ya hali hiyo, wananchi wengi hawaelewi kiendeleacho kila siku serikalini na hawawezi kushiriki kikamilifu katika maisha ya kitaifa.

Kwa hakika wananchi wengi wanaishi bila kujua kinachoendelea maishani mwao. Wanaojua ndio wanaofahamishwa zaidi ilhali wasiojua wanaendelea kudidimia katika wimbi la giza la kutojua. Hali hii inaoana vizuri sana na nadharia ya mwanya wa maarifa inayoelezwa na Oskamp (1991: 181). Nadharia hii inaeleza kuwa watu katika matabaka ya juu ambao wengi tayari ni wasomi na weledi wanaendelea kupokea habari zaidi kutoka kwa vyombo vya habari kuliko wachochole na hivyo kuendelea kuongeza tofauti baina ya makundi hayo mawili. Au tunafanya mengi katika Kiingereza kwa makusudi ili tuweze kuendeleza kutofahamu miongoni mwa umma kwa minajili ya kutaka kuendelea kudhibiti kwa manufaa ya walio na uwezo?

**Uhamasishaji wa Umma katika Maendeleo**

Maendeleo ya jamii, japo yanaelekezwa na serikali na asasi nyingine, ni suala la ushirikiano. Ni lazima serikali ishirikiane na umma katika harakati za kuyaboresha maisha yao. Hili linahitaji ushirikishwaji wa umma katika maandalizi na utekelezaji wa sera mbalimbali za ustawi wa jamii. Ili kuweza kulifikia lengo hilo ni lazima pawe na mfumo ufaao wa mawasiliano baina ya serikali au asasi na mashirika mbalimbali ya maendeleo na wananchi wanaoathiriwa na shughuli za mashirika hayo. Ni sharti wananchi wahamasishwe na kupewa uwezo wa kufanya maamuzi kwa kujua hali mbalimbali zilizopo. Lazima wafahamu mambo muhimu, matukio mageni pamoja na uvumbuzi unaojitokeza katika jamii na jinsi hali hizo zitakavyowaathiri.

Sera na mipango ya serikali katika nyanja za kisiasa, kitamaduni, kiuchumi, kielimu kiafya, n.k zapaswa kuwasilishwa kwa watu kwa lugha ambayo wataielewa. Kwa kufahamishwa awali kuhusu maamuzi mbalimbali yaliyochukuliwa na kujua mapema manufaa na athari zake, wananchi watakuwa tayari kujitoa mhanga katika juhudi za kuleta mabadiliko na maendeleo maishani mwao. Hili halitawezekana iwapo tutaendelea kung'ang'ania matumizi ya lugha isiyoeleweka katika kuandaa na kueleza mipango yetu ya maendeleo. Ung'ang'anizi huo unazua shauku na hali ya kutoaminiana miongoni mwa watu. Kwa mfano, mpango wa baraza la jiji la Nairobi wa kutaka kujenga upya baadhi ya mitaa ya Nairobi lilipokelewa na wengi kwa wasiwasi kwani mpango huo

haukuwekwa wazi na watu wakauelewa. Kipindi cha "Debate" cha 14-09-00 kilichojaribu kuliweka suala hilo wazi katika runinga ya KBC, kililijadili kwa lugha ya Kiingereza na hivyo wakaazi wengi wa maeneo hayo hawakufaidika. Njia nzuri ya kurekebisha hali hii ni kusisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyingine za kienyeji ili kuwafahamisha watu hatua tunazonuia kuzichukua, kwanini, pamoja na manufaa wanayotarajiwa kuyapata kutokana na hatua hizo.

Tumejenga mazoea ya kuyajadili mambo muhimu katika ngazi za kitaifa na kuwaruhusu wasomi kutoa mchango na maoni yao katika magazeti na vyombo vingine vya habari, kwa Kiingereza, kisha maamuzi yanayofikiwa yanatekelezwa kwa nchi nzima. Tunapoendelea kufanya hivyo, wananchi wengi wanakuwa abiria wasioelewa kiendeleacho na kazi yao inabakia kufuata tu maagizo ama kunung'unika kichinichini. Hali hii sharti ibadlike ili sote tuzimiliki harakati za kuendeleza taifa letu. Kuna sababu gani ya kuandaa hotuba nzuri kuhusu masuala muhimu na kuziwasilisha kwenye mkutano wa hadhara huko vivijini katika lugha isiyoeleweka?

Hata kama sote hatuwezi kushiriki moja kwa moja katika kutoa maamuzi mbalimbali, ni lazima tufahamishwe yaliyojadiliwa na yaliyoamuliwa kwani sote tu wahusika katika maendeleo ya nchi hii. Barry et al. (1965: 218) anaeleza kuwa uhusika wa watu katika masuala ya kisiasa unahusiana kwa karibu sana na suala la lugha ambapo matumizi ya lugha moja inayofahamika zaidi huwezesha umma mkubwa kushiriki. Nafikiri hali hii si katika siasa tu bali pia katika masuala ya kiuchumi, kielimu, kiafya na kadhalika. Kwa wakati huu vyombo vya habari vimeendeleza hali ya kuzuia uhusika mkuu wa watu. Tunaelekea kutaka kujenga uhusika mpana kwa kutumia lugha ambayo haieleweki kwa wengi. Tunafanya hivyo kwa matumizi ya ama Kiingereza kwa masuala nyeti au kwa lugha zetu mbalimbali za asili tunapotaka ufuasi finyu wa kikabila. Mwenendo huu unawatenga wengi na sharti urekebishwe. Suluhisho muafaka zaidi lingekuwa ustawi wa lugha zetu za Kiafrika ili zitumike katika nyanja nyingi zaidi. Lugha hizi zikitumika zitatuwezesha kuwafikia watu wote hata wale ambao hawafahamu Kiswahili kwani takribani kila mtu anaijua lugha yake ya asili. Hilo ni gumu zaidi kwa sababu ya gharama. Tunapohimiza matumizi ya Kiswahili kuuhamasisha umma isieleweke kwamba tunataka kuzitupilia mbali lugha nyingine za Kiafrika, la hasha! Tunaamini kuwa zinapaswa kupewa nafasi zaidi.

***Mafao kwa Lugha***

Vyombo vya habari vimetokea kuwa mwalimu mzuri zaidi wa lugha kuliko mwalimu mwingine yeyote kwa sababu ya wingi wa wanafunzi wake (hadhira yote ya vyombo hivyo). Makunja (Mlacha, 1995) anaonya kwamba vyombo

hivyo vinaweza kuendeleza au kuharibu lugha. Naamini kuwa uharibifu waweza kutokea pale tu ambapo lugha haitumiki katika misingi yake sahihi. Kiswahili ni miongoni mwa lugha ambazo zimefaidika sana kutokana na vyombo vya habari ambavyo vimeshiriki katika harakati za kuikuza, kuiendeleza na kuisambaza. Dadi (Mlacha, 1995) anakiri kwamba hapa Afrika Mashariki na Kati, vyombo vya habari viko mstari wa mbele kuendeleza lugha hii. Kuhusu suala hilohilo la lugha na vyombo vya habari, Adegbija (1994:39) anasema:

> Vyombo vya habari vya uchapishaji vimekuwa na athari kubwa ya kuipa lugha sifa na kuiwezesha kujiendeleza na kuifikia hadhira iliyo mbali.

Kwa hakika athari hii inaletwa na vyombo vya habari kwa jumla, wala si vile vya uchapishaji peke yake. Isitoshe, matumizi ya lugha katika vyombo vya habari huipa heba na umaarufu kwa kuiboresha hadhi yake. Kutokana na ukweli huo, matumizi zaidi ya Kiswahili katika vyombo vya habari yatakuwa na manufaa maradufu. Kwanza, tutawafikia wananchi wengi zaidi na kuwahusisha katika mambo yanayoathiri maisha yao. Pili, tutakuwa tunaiendeleza lugha yenyewe na kuiweka tayari kututumikia katika jamii inayobadilika.

**Hitimisho**

Kuingia kwa jamii katika ustaarabu mpya unaoipatia habari nafasi ya msingi maishani kunaelekea kuigawa upya jamii katika matabaka mawili makuu. Kwa upande mmoja wapo wale walio na nafasi nzuri katika nyanja ya habari na mawasiliano kwa jumla, na upande wa chini una wengi ambao hawana habari wala ufahamu wowote kuhusu mkondo unaoongoza maisha yao. Hali hii inaendelezwa zaidi kutokana na kuibuka kwa mitambo mipya ihusianayo na habari, ambayo ni matokeo ya maendeleo makubwa ya uvumbuzi wa kiteknolojia. Yapo mataifa ambayo yanaenda mbio sambamba na uvumbuzi huo na yale maskini ambayo daima yako nyuma kutokana na uwezo wao finyu. Katika nchi zetu maskini, wapo wachache ambao wanapata manufaa ya haya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano lakini idadi kubwa ya wananchi ingali gizani. Hii idadi kubwa itategemea sera ya serikali kuhusu suala la mawasiliano na zaidi kupitia vyombo vya habari vya umma.

Ili wananchi wengi washirikishwe katika kuiandaa hatima ya nchi yao na waweze kufaidi manufaà ya wimbi hili la jamii kuwa "jamii ya habari," ni lazima hatua zichukuliwe kuirekebisha sera iongozayo suala la mawasiliano kwa umma. Tatizo kubwa ambalo tumelionyesha ni kwamba kwa kiasi kikubwa hatuwasiliani na watu. Ni wachache tu ambao wanafahamu vyema yanayowazunguka. Ni lazima suala la lugha itumiwayo katika vyombo vya habari vya umma na vya kibinafsi irekebishwe. Tusiendelee kufikiri kuwa kuna kundi la wachache wafaao kuelezwa yanayojiri na kuulizwa maoni yao na wengi

ambao wanasubiri gizani kuitikia tu na kutekeleza maamuzi ya wakubwa. Wananchi wote wana haki ya kimsingi ya kufahamishwa.

**Marejeo**


Adegbija, E. (1994), *Language Attitudes in Sub Saharan Africa, A Sociolingustic Overview*. Clevedon, Philadelphia & Adelaide: Multilingual matters

Barry, G., Bronowski, J., Fisher, J., Huxley, J. (eds.), (1965), *Communication and language:Networks of Thought Action*. London: Macdonald.

Dadi, K.S. (1995), "Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Msamiati," Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo Vya Habari*, Dar es Salaam: TUKI.

Dicard, W.P. (1982), *The Coming Information Age*. New York and London: Longman.

Kasamu, R.N. (1996), "The Role of Information in Industrial Development-The Case of Engineering Development and Service Centre (EDCS)", KIRDI National Workshop on the Role of Industrial and Technological Information in Industrial Development

Kiganya, W. (1995), " Sera ya Kiswahili, Mafaniko na Matatizo nchini Kenya", Mlacha (mh.), *Kiswahili katika Kanda ya Afriki Masharki*, Dar es Salaam: TUKI

Lumumba, K.T. (1997), "Information Superhighway: Its potential as a tool for Information Dissemination", ARCEDEM/KIRDI sensitization lecture on Information Acquisition/Dissemination for Industrial Growth

Lyon, D. (1988), *The Information Society, Issues and Illusions*. Cambridge: Polity press

Mberia, K.W. (2000), " Kiswahili and Other Indigenous Languages in Performing Arts", Makala ya National Drama Training workshop 2000, *Performing Arts for National Development*. Kenyatta University, 21-25 Aug 2000.

McQuail, D. (1987), *Mass Communication Theory*, London: Sage Publications Ltd.

Mlacha, S.A.K. (Mh.), (1995), *Kiswahili na Vyombo vya Habari*, Dar es Salaam: TUKI

Mlacha, S.A.K. (Mh.), (1995), *Kiswahili Katika Kanda ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: TUKI

Oskamp, S. (1991) *Attitudes and Opinions*. Englewood cliffs, New Jersey: Prentice Hall

Osoro, J. (2000), "Just Shout Back," *Daily Nation*, 30th , June

Osoro, J. (2000), "Radio Regains its Glory," *Daily Nation*, 30th , June

Wood, D.N. (1983), *Mass Media and the Individual*, Minnesota: West Publishing Company